TANGAZO LA SERIKALI NA. 237 la tarehe 24/3/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa Chini ya Kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA ISHINABULANDI YA MWAKA, 2023

Jina:

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Ishinabulandi ya mwaka, 2023

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji (mpango wa urasimishaji) kwa madhumuni ya Sheria ya Mipango Miji.

Mpango katika eneo la kwenye Jedwali

3. Mipango ya Jumla na kina kwa eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga.

*Tangazo la Serikali Na. 237 (Liandelea.)*

JEDWALI

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:-

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 540876.667MS, 9585362.019KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki - Kaskazini katika uelekeo wa KZ57º57'49.64''MG kwa umbali wa lilometa 2.79 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 543242.044MS, 9583881.888KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa KZ33º36'53.55''MG kwa umbali wa kilomita 0.94 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba C yenye majira - nukta 542724.175MS, 9583102.872KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa KZ59º22'15.06''MS kwa umbali wa kilomita 1.35 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 541560.962MS, 9583791.593KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini – Magharibi katika uelekeo wa KZ33º49'46.24''MS kwa umbali wa kilomita 0.91 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 541055.487MS, 9583037.363KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki katika uelekeo wa KS83º35'52.32''MS kwa umbali wa kilomita 2.44 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F yenye majira - nukta 538632.442MS, 9583309.243KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KS37º09'38.69''MG kwa umbali wa kilomita 1.11 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba G yenye majira - nukta 538632.442MS, 9583309.243KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki - Kusini katika uelekeo wa KZ61º41'08.80''MG kwa umbali wa kilomita 0.76 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H yenye majira - nukta 538632.442MS, 9583309.243KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ30º26'01.30''MG kwa umbali wa Kilomita 1.18 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
6 Februari, 2023

BANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*